

HALMASHAURI YA WILAYA YA MUHEZA
(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Simu Na: 027 2641105
Mtendaji



Ofisi ya Mkurugenzi

Wilaya ya Muheza
S. L. P. 20
MUHEZA

Fax Na: 027 2641414

Kumb.NA.MUH/S.80/14/102
03/10/2019

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA MUHEZA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza anawatangazia wananchi wote wenyе sifa kuomba nafasi ya kazi ya Mkataba wa mwaka mmoja kwa nafasi 01 ya fundi sanifu (magari).

1. FUNDI MAGARI (NAFASI 01)

Sifa za Muombaji:-

- (a) Wenye elimu ya kidato cha nne (IV) au kidato cha sita (VI)
- (b) Awe amehitimу mafunzo ya fundi sanifu magari, katika Daraja/Grade I au ngazi Daraja la III na oridinary diploma
- (c) Awe na umri usiozidi miaka 45

2. Masharti ya Jumla kwa waombaji

- (a) Mwombaji awe Mtanzania
- (b) Asiwe amewahi kutiwa hatiani kwa kosa la jinai
- (c) Asiwe amewahi kufukuzwa kazi Serikalini
- (d) Maombi yote yaambatanishwe na maelezo binafsi ya mwombaji (CV) na wadhamini wawili na namba zao za simu
- (e) Maombi yote yaambatanishwe na vivuli vya vyeti vya kumaliza shule na mafunzo
- (f) Waombaji wote wanatakiwa kuwa na vyeti vya kuzaliwa
- (g) Maombi yawe na anuani kamili pamoja na namba za simu ili kurahisisha mawasiliano
- (h) Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 18/10/2019 saa 09.30 alasiri
- (i) Waombaji wenyе sifa wataitwa kwenye usaili
- (j) Mwombaji ni lazima awe Raia wa Kitanzania.

Kazi na Majukumu ya fundi magari:-

- (a) Kufanya ukaguzi wa ubora wa magari ya Serikali na kerekebisha ipasavyo.
- (b) Kufanya upimaji wa Mitambo na Umeme kufuatana na umeme na maelekezo ya Mhandisi.
- (c) Kufanya kazi za kutengeneza mitambo, magari na vifaa vya umeme;
- (d) Kufanya usanifu wa miradi midogo midogo ya umeme;

Kusimamia jinsi ya kufunga mashine mpya zinazowekwa kwenye karakana za ufundu na Umeme
(e)Kufanya ukaguzi wa matengenezo ya mitambo,magari.

Ngazi ya Mshahara

Ngazi ya Mshahara kwa cheo hiki ni Tshs. TGS C1 525,000/= kwa mwezi.

Maombi yote yatumwe kwa

MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA,
HALMASHAURI YA WILAYA,
S.L.P 20,
MUHEZA.